JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

---

SHERIA YA MTOTO

[SURA YA 13]

# TAFSIRI YA KANUNI ZA KANUNI ZA MAFUNZO YA UANAGENZI ZA MWAKA 2012

Toleo hili la Kanuni za Mafunzo ya Uanagenzi za mwaka 2012, Tangazo la Serikali Na. 153 la Tarehe 4 Mei, Mwaka 2012, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam
28 Aprili, 2016

GEORGE M. MASAJU,
*Mwanasheria Mkuu Wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 172 la tarehe 13/05/2016

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

---

# KANUNI ZA MAFUNZO YA UANAGENZI ZA MWAKA 2012

## SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

## SEHEMU YA PILI
MAFUNZO RASMI YA UANAGENZI NA MAFUNZO YA UANAGENZI YASIYO RASMI

4. Kutolewa kwa mafunzo ya uanagenzi.
5. Mafunzo rasmi ya uanagenzi.
6. Mafunzo ya uanagenzi yasiyo rasmi.

## SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA CHINI YA MAFUNZO YA UANAGENZI

7. Umri wa chini kuhusu mafunzo ya uanagenzi.
8. Ridhaa ya mwangalizi kuhusu mafunzo ya uanagenzi ya mtoto.
9. Ridhaa ya mtoto kuhusu mafunzo ya uanagenzi.
10. Kiwango cha chini cha mafunzo ya uanagenzi.

## SEHEMU YA NNE
KATAZO LA KUWA NA MAZINGIARA HATARISHI KWENYE MAFUNZO

11. Katazo la kuwa na mazingira hatarishi kwenye sehemu ya mafunzo.

SEHEMU YA TANO
WAJIBU WA MTOA MAFUNZO YA UANAGENZI

12. Mafunzo ya maandalizi ya kazi ya baadaye ya mwanagenzi.
13. Mahudhurio na mafunzo ya uanagenzi.
14. Wajibu wa kutoa cheti cha mafunzo.
15. Ulinzi wa mwanagenzi dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji.
16. Usajili wa mwanagenzi.

SEHEMU YA SITA
MAKUBALIANO YA MAFUNZO YA UANAGENZI

17. Makubaliano kutiwa saini ya mtoa mafunzo na mwangalizi wa mtoto.
18. Kusitishwa kwa makubaliano ya mafunzo ya uanagenzi na mtoa mafunzo.
19. Kusitishwa kwa makubaliano ya mafunzo ya uanagenzi na mwangalizi wa mtoto.
20. Wajibu wa mwangalizi wa mtoto kutoa taarifa za kunyanyaswa au kuonewa/kunyonywa.
21. Kukiukwa kwa mkataba/ makubaliano ya mafunzo ya uanagenzi.

SEHEMU YA SABA
MAJUKUMU YA MWANAGENZI NA MWANGALIZI

22. Wajibu wa mwangalizi wa mtoto kutoa taarifa za kunyanyaswa au kuonewa/kunyonywa.
23. Wajibu wa kufuata maelekezo halali.
24. Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu uharibifu wa mali.
25. Wajibu wa mtoto kutoa taarifa kuhusu kunyanyaswa au kunyonywa.
26. Wajibu wa mtoto kutoa taarifa kuhusu kunyanyaswa au kunyonywa.

SEHEMU YA NANE
USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI

27. Wajibu wa Afisa Kazi.
28. Wajibu wa Msimamizi wa Elimu ya Ufundi.
29. Wajibu wa Afisa Ustawi wa Jamii.
30. Wajibu wa Mkaguzi wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

## SEHEMU YA TISA
### UTATUZI WA MIGOGORO

31. Adhabu kwa ukiukwaji.
32. Utatuzi wa migogoro.

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

# KANUNI

KANUNI ZA MAFUNZO YA UANAGENZI ZA MWAKA 2012

## SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Mafunzo ya Uanagenzi chini ya Sheria ya Mtoto, za mwaka, 2012.

Matumizi

Sura 82
Sura 82, 366 na 13

**2.** Kanuni hizi zitatumika kwa Wizara zote, Wakala za Serikali na Idara pamoja katika vyombo vingine au na watu binafsi wanaotoa mafunzo ya uanagenzi nchini Tanzania na zitasomwa pamoja na Sheria ya Elimu ya Ufundi Stadi na Sheria ya Mahusiano Kazini na Sheria nyingine zozote zinazohusika na Kanuni.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"sheria" maana yake ni Sheria ya Mtoto ya Tanzania;

"mafunzo rasmi ya uanagenzi" maana yake ni mchakato wa kutoa mafunzo ya ujuzi au weledi wa kazi unaoweza kutolewa chuoni au mahali pa kazi kwa kutumia sekta rasmi au isiyo rasmi;

"mwanagenzi" maana yake ni mtoto aliye na umri wa miaka kumi na mine au zaidi ambaye ameajiriwa ili kujifunza ujuzi katika sekta rasmi au isiyo rasmi;

"mwangalizi" maana yake ni mzazi, mlezi, au idara iliyopewa mamlaka ya kuangalia mtoto, kiongozi wa kijiji au kamati ya kijiji inayotambuliwa rasmi kwa ajili hiyo, mwalimu au mtu yeyote anayewajibika kumwangalia mtoto;

"mtoto" maana yake ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane;

"kazi hatarishi" maana yake ni kazi yeyote inayomweka mtoto katika hatari ya kimwili au kiakili;

"afisa wa kazi" maana ni afisa aliye na majukumu ya ukaguzi mahali pa kazi kama inavyoelekezwa kwa mujibu wa kifungu cha 43 kifungu kidogo cha (3) cha Sheria ya Mahusiano Kazini;

Sura 300

"mtu mwenye ulemavu" maana yake ni mtu mwenye ulemavu wa mwili au akili, ambaye uwezo wake wa kufanya kazi unakuwa mdogo anapokumbana na vikwazo vya hisia, mazingira na kitaasisi;

"ujira" maana yake ni jumla ya thamani ya malipo yote ya kifedha ambayo anayestahili kulipwa mwanagenzi kutokana na kazi iliyofanywa wakati wa kipindi cha mafunzo ya uanagenzi;

"Afisa Ustawi wa Jamii" maana yake ni Afisa Ustawi wa Jamii aliye katika utumishi wa umma;

"mtoa mafunzo" maana yake ni mwajiri au taasisi yeyote iliyosajiliwa au mtu anaye wajibika kutoa mafunzo ya uongozi kwa mujibu wa sheria za ndani na viwango;

"viwango vya usalama wa afya kazini" ina maana iliyotolewa kwake chini ya Sheria ya Usalama wa Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297.

## SEHEMU YA PILI
## MAFUNZO RASMI YA UANAGENZI NA MAFUNZO YA UANAGENZI YASIYO RASMI

Kutolewa kwa mafunzo ya uanagenzi

**4.** Mafunzo ya Uanagenzi yatatolewa kwa sekta rasmi na isiyo rasmi kwa mujibu wa Kanuni zilizotugnwa na taasisi zinazohusika na mafunzo ya uanagenzi.

Mafunzo rasmi ya uanagenzi

**5.-**(1) Kutakuwa na mafunzo ya kijasiriamali na mafunzo rasmi yanayotolewa kitaasisi.

(2) Mafunzo yanayotoewa chini ya taasisi iliyosajiliwa chini ya Mamlaka iliyo na dhamana na mafunzo ya ufundi stadi.

(3) Mafunzo ya kijasiriamali yatatolewa na taasisi za kijasiriamali kwa kushirikiana na taasisi zinazotoa mafunzo rasmi ndani na nje ya nchi chini ya masharti yaliyoainishwa kwenye makubaliano baina ya taasisi ya kijasiriamali, mtoa mafunzo na

mamlaka husika ya Serikali.

(4) Mtoa huduma atatakiwa, kwa kiwango cha chini kabisa, kuwa na yafuatayo:

(a) vifaa vya kufanyia kazi na vifaa vya kujikinga kwa ajili ya wanagenzi;
(b) vifaa salama na safi vya choo kwa ajili ya wanagenzi;
(c) mahali pa mapumziko kwa ajili ya wanagenzi kujipumzisha wakati wa kipindi cha mapumziko; na
(d) mazingira salama kwa ajili ya wanagenzi kufanyia mafunzo.

(5) Taasisi za kijasiriamali zinazotoa elimu ya ufundi stadi zinaweza kupewa ruzuku kwa kadri ambavyo Serikali itaona inafaa.

(6) Wanagenzi walio na uwezo wa kusoma na kuandika walio na kiwango cha chini kabisa cha elimu kwa kadri itakavyoainishwa na mamlaka ya Serikali inayohusika na utolewaji wa elimu ya ufundi stadi watakuwa na sifa za kujiunga na mafunzo rasmi ya uanagenzi.

(7) Mafunzo rasmi ya uanagenzi yatafanywa na taasisi iliyoidhinishwa kutoa mafunzo hayo kwa ngazi iliyotajwa na mamlaka husika ya Serikali.

(8) Mafunzo ya uanagenzi yanayotolewa na taasisi ya kijasiriamali yatatolewa chini ya masharti yanayosimamiwa na msimamizi aliye na sifa kutoka katika taasisi ya kijasiriamali inayosimamiwa na mamlaka husika ya Serikali.

(9) Mtoa mafunzo atashauri katika kila hatua ya mafunzo kuhusiana na yaliyomo katika mafunzo, mfumowa ufundishaji na masuala mengine kuhusiana na mafunzo hayo.

(10) Maombi ya kupata mafunzo rasmi ya uanagenzi yanaweza kufanywa na mwajiri kwa niaba ya mwanagenzi, watu au wanafunzi wa mafunzo ya ufundi stadi (VETA) ambao wamemaliza ngazi zilizoidhinishwa za mafunzo kwa ukamilifu au kwa kadri ambavyo viwango vya elimu ya ufundi stadi vitaainisha na kwa namna ilivyoainishwa na mamlaka husika ya Serikali iliyo na dhamana na masuala ya elimu ya ufundi stadi.

(11) Taasisi zinazotoa mafunzo rasmi zitatumia mtaala uliowekwea na taasisi husika kwa ajili ya kuelekeza utolewaji husika kwa ajili ya kuelekeza utolewaji wa mfumo rasmi wa mafunzo.

(12) Mafunzo yanayotolewa na sekta rasmi yatakidhi masharti ya Sheria na kanuni kuhusiana na haki za watoto.

(13) Mwanagenzi anayetoka kwenye familia iliyo na kipato cha chini anayepata matatizo ya kulipa ada au malipo mwengine yanayohusiana na gharama za masomo, atasaidiwa kupata msaada wa kifedha na mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sekta binafsi au watu kwa kushirikiana na mwangalizi wa mtoto.

Mafunzo ya uanagenzi yasiyo rasmi

**6**.-(1) Mafunzo yasiyo rasmi ya ufundi yanaweza yakafanywa na chuo chochote au mtu binafsi bila kujali kama ana cheti au hana cheti kwa ajili ya kufanya mafunzo hayo.

(2) Vyuo ambavyo vina vyeti au vimeidhinishwa kutoa mafunzo ya ufundi vitatoa mafunzo hayo kwa kuzingatia sheria ndogo na kanuni kuhusu viwango na ngazi ya mafunzo kama ambavyo itakuwa imeelekezwa na taasisi husika ya Serikali.

(3) Taasisi husika ya Serikali itaamua sifa za chini za kwa ajili ya mwanagenzi kuanza mafunzo yasiyo rasmi kwa mtoto ambaye amefikisha kiwango cha chini cha elimu inayotakiwa.

(4) Mafunzo ya ufundi katika shule ambazo haziko katika mfumo rasmi yatafanyika kwa kipindi kisichozidi miaka minne.

(5) Hakuna kiwango cha chini cha sifa za kuanza mafunzo ya ufundi iwapo mtoto anayetakiwa kupata mafunzo hayo hajahitimu elimu ya msingi ambayo ni ya lazima.

(6) Mwanagenzi katika kipindi atakapokuwa anapatiwa mafunzo katika vyuo ambavyo siyo rasmi atastahili kulipwa posho ya kujikimu ambayo itapangwa kwa makubaliano kati ya mtoa mafunzo na mwangalizi wa anayemtunza mtoto.

(7) Mtoa mafunzo ya ufundi atakuwa akiangaliwa katika kila hatua ya mafunzo kuhusu maudhui ya mafunzo, ya ufundishaji na mambo mengine yeyote yanayohusu kufundisha.

(8) Maombi kwa ajili ya kufanya mafunzo yasiyo rasmi ya ufundi yatafanywa na anayemtunza mtoto, mwajiri kwa niaba yake au watoto wenyewe binafsi kwa uangalizi au uongozi wa mwangalizi wa mtoto.

(9) Vyuo vilivyothibitishwa kwa ajili ya mafunzo ya ufundi yasiyo rasmi watatumia mitaala ya viwango vilivyowekwa mahsusi na taasisi zinazohusika kwa ajili ya kuwasaidia katika kutoa mafunzo na kuzingatia sheria zote zinazohusu haki za mtoto.

(10) Mwanagenzi ambaye anatoka katika familia yenye

kipato cha chini na ambaye anapata matatizo kulipa ada au malipo mengine yanayohusiana na masomo, atasaidiwa kupata msaada wa kifedha na Serikali za Mitaa, shirika binafsi au mtu binafsi kwa kushirikiana na mwangalizi wa mtoto.

(11) Mwanagenzi baada ya kutimiza miaka minne akipatiwa mafunzo ya ufundi, atahesabiwa kuwa na ujuzi au weledi sawa kama wa mwanagenzi aliyepata mafunzo katika chuo rasmi cha mafunzo ya ufundi.

## SEHEMU YA TATU
### MASHARTI YA CHINI YA MAFUNZO YA UANAGENZI

Umri wa chini kuhusu mafunzo ya uanagenzi

**7.-**(1) Umri wa chini wa kujiunga na mafunzo ya uanagenzi utakuwa ni miaka kumi na nne.

(2) Mtoto wa miaka kumi na minne ambaye bado anahudhuria elimu ya lazima hatakuwa mwanagenzi hadi hapo atakapomaliza miaka ya lazima ya shuleni.

(3) Mtoto wa miaka mine na zaidi aliyemaliza elimu ya msingi ya lazima anaweza kujiunga na mafunzo yasiyo rasmi ya uanagenzi.

Ridhaa ya mwangalizi kuhusu mafunzo ya uanagenzi ya mtoto

**8**.-(1) Mwangalizi atatakiwa kuridhia mafunzo ya uanagenzi kabla ya mtoto kujiunga na uanagenzi.

(2) Mtoa mafunzo atamtaarifu mwangalizi kuhusu vigezo na masharti ya uanagenzi na kipekee kuhusiana na ujuzi uliotolewa na wajibu uliowekwa kwa mtoto au mwangalizi.

Ridhaa ya mtoto kuhusu mafunzo ya uanagenzi

**9.-**(1) Mtoa mafunzo atamtaarifu mwangalizi kuhusu vigezo na masharti ya uanagenzi na kipekee kuhusiana na ujuzi uliotolewa na wajibu uliowekwa kwa mtoto au mwanagenzi.

(2) Mtoto atapewa nafasi ya kutafakari taarifa iliyotolewa kabla ya kutoa uamuzi wa mwisho.

(3) Mtoa huduma atakuwa na wajibu wa kumhoji mtoto na kujiridhisha pasipo kuacha shaka kuwa mtotoameridhia na anakusudia kufanya mafunzo ya uanagenzi.

(4) Mtoto atatakiwa kuonyesha ridhaa yake kwa maandishi kwa kutoa ridhaa kwa mtoa mafunzo mbele ya mwangalizi wake.

Kiwango cha chini cha mafunzo ya uanagenzi

**10.-**(1) Mamlaka ya Serikali iliyo na dhamana na masuala ya ufundi stadi itaweka viwango vya wanagenzi kwa kila fani kwa kuzingatia usalama na ustawi wa mtoto.

(2) Masaa ya juu ya mafunzo kwa wiki hayatazidi masaa thelathini na sita.

(3) Masaa ya juu ya mafunzo kwa wiki hayatazidi masaa thelathini na sita.

(4) Mtoto hatafanya mazunzo kati ya masaa ya saa mbili usiku na saa kumi na mbili asubuhi.

(5) Mtoto hataruhusiwa kufanya mafunzo zaidiya muda uliotajwa na kanuni hizi.

(6) Mtoto aliye kati ya miaka kumi na minne na miaka kumi na sita hatabeba mizigo inayozidi kilogramu kumi na iwapo ni mtoto wa miaka kumi na sita hadi kumi na minane, mzigo wa kilogramu ishirini, isipokuwa kwamba afisa kazi au mganga atakuwa na mamlaka ya kupunguza uzito ulioruhusiwa pale ambapo mtoto ana tatizo linalotambulika.

(7) Mtoto hatahudhuria mafunzo ya uanagenzi kwa zaidi ya siku sita katika wiki moja na kwenye sikukuu.

(8) Mtoto ambaye anafanya kazi kwa zaidiya masaa matatu kwa siku moja atapewa chakula au kipindi cha mapumziko cha angalau saa moja

(9) Mtoto atatakiwa kupewa likizo ya siku thelathini ili kuwa mbali na eneo la mafunzo ya uanagenzi.

(10) Mafunzo yaliyotolewa yatahakikisha kuwa mwanagenzi anakingwa dhidi ya matumizi ya vifaa vinavyohatarisha usalama wake.

(11) Mtoa mafunzo atahakikisha kuwa mwanagenzi hapatiwi nafasi ya uingiaji bila ya kuwa chini ya uangalizi au kutakiwa kufanya kazi kwenye mashine zisizokuwa chini ya uangalizi ambazo zinaweza kuhatarisha afya na usalama wake.

(12) Mtoa huduma atahakikisha kuwa mwanagenzi anatumia mavazi ya kazi na nyenzo nyingine salama.

## SEHEMU YA NNE
### KATAZO LA KUWA NA MAZINGIRA HATARISHI KWENYE MAFUNZO

Katazo la kuwa na mazingaira hatarishi kwenye sehemu ya mafunzo

**11.-**(1) Kazi, kwa mukhtadha wa uanagenzi, inachukuliwa kuwa ni aina mbaya kabisa ya ajira ya mtoto pale ambapo mwanagenzi aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane anahusishwa na aina au mazingira hatarishi ya kazi ndani ya uangalizi unaostahili.

(2) Mtoto hatatakiwa kufanya kazi ya uanagenzi bila ya idhini na usimamizi wa chombo cha Serikali kilichoidhiniwa katika yoyote kati ya shughuli zijulikanazo kama "kazi hatarishi" chini ya kifungu cha 28 cha Serhai au Kanuni zozote zilizotungwa chini ya Sheria au chini ya Sheria ya Usalama wa Afya Mahali Pa Kazina Kanuni zozote zilizotungwa chini ya Sheria hiyo au Sheria nyingine na Kanuni zake.

(3) Kwa madhumuni ya uelewa, "kazi hatarishi" zitajumuisha kazi zote ambazo zinaweza kumdhuru au kumuweka mtoto hatarini kimwili au kumsababishia majeraha ya kiakili na zinajumuisha shughuli zote zilizoainishwa kwenye orodha ya kazi hatarishi iliyoambatanishwa kwenye Kanuni za Ajira ya Mtoto.

(4) Mtoa mafunzo atazingatia Sheria na Kanuni zinazosimamia ajira ya mtoto.

(5) Mtoto hatapatiwa mafunzo kwenye mazingira yanayosababisha hatari ya afya na usalama wake, ikijumuisha kufanya kazi inayohusiana na vumbi au moto, kemikali hatarishi, kelele zilizozidi kiwango, mtetemeko, joto, kuinama, kusimama au kukaa chini, kuwekwa kwenye mazingira ya pombe au kwenye mazingira yenye ubichi uliozidi, vifaa vya kazi hatarishi kama mashine nzito, kubeba mizigo mizito mgongoni, kichwani au mabegani na kitendo kingine chochote ambacho kinaweza kuathiri afya na usalama wa mtoto.

(6) Mwanagenzi hatajihusisha na kazi yoyote au mafunzo ambayo yanahusiana na matendo ya kujamiiana, yanayomuweka kwenye mazingira ya kingono au yaliyo kinyume na maadili na picha na mikanda ya video ya utupu.

## SEHEMU YA TANO
### WAJIBU WA MTOA MAFUNZO YA UANAGENZI

Mafunzo ya maandalizi ya kazi ya baadaye ya mwanagenzi

**12.-**(1) Mtoa mafunzo atatoa mafunzo ya awali kuhusiana na fani kwa mtoto kabla mtoto hajaanza mafunzo.

(2) Mafunzo ya awali kuhusiana na fani yatajumuisha, isipokuwa hayatakuwa na ukomo kuhusiana na faida na hasara za biashara, hatari na changamoto.

(3) Kwa madhumuni ya ufundishaji unaofaa, mtoa mafunzo anaweza akatoa msaada wa kisaikolojia jamii, ushauri nasaha na mwongozo pale inapohitajika na mtoto kulingana na uhitaji na mazingira ya kila mtoto.

(4) Pale ambapo mtoa mafunzo anashindwa kutoa msaada wa kisaikolojia, ushauri nasaha au muongozo, atampeleka mtoto kwa Afisa Stawi wa Jamii au taasisi nyingine iliyoidhinishwa.

Mahudhurio na mafunzo ya uanagenzi

**13.-**(1) Mtoa huduma atawajibika kuhakikisha kuwa mahudhurio ya wanagenzi ni ya mara kwa mara kwa kuweka kitabu cha mahudhurio ambacho wanagenzi watatakiwa kusajili mahudhurio yao kwa kila siku.

(2) Mtoa mafunzo katika vyuo rasmi atawajibika kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kuhusiana na biashara kama ilivyoainishwa na mamlaka iliyo na dhamana na mafunzo ya ufundi stadi.

(3) Mtoa mafunzo katika sekta rasmi atawajibika kutoa mafunzo kwa vitendo na mafunzo mengine kwa kadri ambavyo mazingira yanahitaji.

(4) Mtoa mafunzo katika sekta rasmi na zisizo rasmi atawajibika kutoa taarifa kuhusiana na soko la biashara, kuuzika kwa bidhaa, ujasiriamali, maisha na muongozo kwa ajili ya sekta rasmi na isiyo rasmi.

Wajibu wa kutoa cheti cha mafunzo ya ufundi

**14.-**(1) Mtoa mafunzo katika sekta rasmi atawajibika kumpatia mwanagenzi mtihani unaofaa kwa ajili ya sekta rasmi na kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na mamlaka husika ya Serikali au mamlaka husika zisizo za kiserikali.

(2) Watoa mafunzo waliosajiliwa katika sekta rasmi watatoa vyeti kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa, mifumo na taratibu kama zilivyowekwa na asasi za kibiashara kwa

kushirikiana na mamlaka zilizo na dhamana ya masuala ya mafunzo ya ufundi stadi.

(3) Cheti cha kuhitimu mafunzo kitaelekeza kuhusu ujuzi na mafunzo yaliyopatikana wakati wa kipindi cha mafunzo.

(4) Msaada wa kisaikolojia, ushauri nasaha na muongozo kwa ajili ya sekta rasmi na isiyo rasmi vitasimamiwa na kuongozwa na mamlaka ya Serikali iliyo na dhamana na mambo ya ustawi wa jamii.

Ulinzi wa mwanagenzi dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji

**15.-**(1) Mtoa mafunzo ya ufundi atahakikisha kuwa mtoto anapata huduma ya afya mara moja iwapo ataumia wakati wa mafunzo.

(2) Mtoa mafunzo atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mwanagenzi haendeshe mashine hatarishi au kufanya kazi kwa kutumia vifaa vingine hatarishi au katika hali yoyote ile, kufanya kazi kwenye mazingira hatarishi.

(3) Mtoa huduma atahakikisha kuwa mwanagenzi anafanya kazi chini ya mazingira salama, ikijumuisha kuhakikisha kuwa wana vitendea kazi au kuchukua hatua nyingine salama ili kuhakikisha usalama dhidi ya madhara au majeraha.

(4) Mtoa mafunzo atamlinda mtoto dhidi ya madhara yoyote wakati wa kipindi cha mafunzo, ikijumuisha madhara ya kisaikolojia (Psychosocial), kiakili, kimwili au mazingaira ambayo yanaweza kumpelekea mwanagenzi kunyanyaswa, kudharauliwa, kuteswaau matendo mengine yaliyo na madhara.

(5) Mtoa mafunzo hatawanyanyasa wanagenzi kwa misingi ya jinsia, kabila, ulemavu, hali ya kuwa na maambukizi ya virusi vya ukimwi, kuwa yatima au hali nyingine yoyote ile.

(6) Mtoa mafunzo katika sekta rasmi atakuwa na jukumu la kutoa sehemu ya mafuunzo inayofaa na chakula kinachofaa na cha kutosha kwa mwanagenzi kwa kipidi cha mafunzo.

(7) Mtoa mafunzo katika sekta rasmi anaweza kufanya majadiliano na muangalizi na mwanagenzi kwa ajili ya kupata mahali panapofaa na chakula cha kutosha kwa mwanagenzi.

(8) Mtoa mafunzo katika sekta rasmi anaweza kufanya majadiliano na muangalizi na mwanagenzi kwa ajili ya kupata mahali panapofaa na chakula cha kutosha kwa mwanagenzi.

(9) Mtoa mafunzo atatoa huduma za choo kwa ajili ya wanagenzi wa kike na wa kiume wakati wa kipindi cha mafunzo.

(10) Mtoa huduma atawajibika kumfichia mwanagenzi pale ambapo amepata jeraha wakati wa mafunzo ya wanagenzi kwa mujibu wa masharti yaliyokubalika na vigezo kwa mujibu wa sheria zinazosimamia masuala ya fidia.

(11) Mtoa mafunzo atahakikisha kuwa mwanagenzi hasababishi tishio lolote au madhara kwa wanagenzi wengine wanaohudhuria mafunzo.

(12) mtoa mafunzo atakidhi masharti ya Sheria na kanuni kuhusiana na usalama wa mtoto.

(13) Baada ya kumaliza mafunzo, mtoa mafunzo atamuondolea mwanagenzi jukuju lolote au wajibu kuhusiana na mtoa mafunzo.

Usajili wa mwanagenzi

**16.-**(1) Mtoa mafunzo atawajibika kuwasajili watoto wote wanaoshiriki katika mafunzo ya uanagenzi.

(2) Rejesta itajumuisha jina na umri wa mtoto, ulemavu wowote, jinsia, makazi, majina ya muangalizi na anuani zake na aina ya mafunzo yatakayotolewa.

(3) Mtoa mafunzo atahakikisha kuwa mawasiliano ya mara kwa mara na muangalizi kuhusiana na maendeleo ya mwanagenzi ikijumuisha kuingiza taarifa mpya kuhusiana na mtoto.

## SEHEMU YA SITA
### MAKUBALIANO YA MAFUNZO YA UANAGENZI

Makubaliano kutiwa saini ya mtoa mafunzo na mwangalizi wa mtoto

**17.-**(1) Kila mtoa mafunzo atatakiwa kusaini mkataba na mwangalizi wa mwanagenzi kabla mwanagenzi hajaandikishwa kwa ajili ya mafunzo.

(2) Makubaliano yataainisha haki na wajibu wa mtoa mafunzo na mwanagenzi.

(3) Kutakuwa na fomu inayoelezea yaliyomo katika mkataba kama ambavyo itakuwa imeainishwa katika Kanuni za Elimu ya Ufundi, utatumika kama mwongozo katika mahusiano ya kimkataba kati ya mtoto na mtoa mafunzo.

(4) Fomu inayoainisha yaliyomo kwenye makubaliano kama ilivyoelezewa kwenye Kanuni za Mafunzo ya Ufundi Stadi, inaweza kutumika kutoa mwongozo kwa mahusiano ya kimkataba baina ya mwanagenzi na mtoa mafunzo.

(5) Mtoa mafunzo kwenye sekta rasmi atafungwa na makubaliano baina ya mwangalizi na mtoa mafunzo au Kanuni nyingine, taratibu au mifumo iliyowekwa na Asasi za Kibiashara.

Kusitishwa kwa makubaliano ya mafunzo ya uanagenzi na mtoa mafunzo

**18.-**(1) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia, kusitishwa kwa uanagenzi kunaweza kufanyika chini ya mazingira yafuatayo pekee:

(a) kutokuwa na uwezo uliothibitishwa na taarifa ya mganga;
(b) kutokuwa na uwezo uliothibitishwa na taarifa ya mganga;
(c) utovu wa nidhamu uliokithiri;
(d) afya duni inayozuia utekelezaji ulio na tija;
(e) masharti ya kiuendeshaji; na
(f) kutokuwa na uwezo wa kujifunza.

(2) Mtoa mafunzo ya atathibitisha kuwa mwanagenzi hana sifa za kuendelea na mafunzo ya uanagenzi.

(3) Mtoa mafunzo, iwapo mkataba umevunjika, atatoa notisi ya siku thelathini kwa mwangalizi na mwanagenzi akiwataarifu kuhusu kuvunjika huko kwa mkataba na sababu ya kuvunjika huko.

(4) Iwapo mwangalizi wa mtoto hawajaridhika na kuvunjika huko kwa mkataba, wataomba msaada wa Afisa Ustawi wa jamii au Afisa Kazi ndani ya kipindi kisichozidi mwezi mmoja kutokea tarehe ya kuvunjika.

Kusitishwa kwa makubaliano ya mafunzo ya uanagenzi na mwangalizi wa mtoto

**19.-**(1) Mwangalizi anaweza kuvunja mkataba kwa niaba ya mtoto iwapo mtoa mafunzo amekiuka mkataba kwa namna yoyote ile.

(2) Mwangalizi wa mtoto atasitisha mkataba baada ya kuwasiliana na mtoto mwenyewe na akijiridhisha kuwa kusitisha mkataba ni kwa manufaa ya mtoto.

(3) Pale ambapo kuvunjika kwa mkataba kunapelekea unyenyasaji wa mtoto, mwanaglizi atamtaarifu Afisa Ustaw wa Jamii ambaye atachukua hatua zote kumuunganisha mtoto na uangalizi stahili.

Wajibu wa mwangalizi wa mtoto kutoa taarifa za kunyanyaswa au kuonewa/ kunyonywa

**20.-**(1) Mwangalizi aliyeko katika sekta rasmi atastahili kupewa malipo kwa namna iliyoainishwa na sheria ya mafunzo ya ufundi stadi na marekebisho yake na Kanuni zilizotungwa chini yake.

(2) Iwapo mtoa mafunzo anashindwa kumlipa mtoto, sheria, kanuni na taratibu za mamlaka husika ya Serikali iliyio na dhamana na mambo ya mafunzo ya ustadi wa jamii vitatumika.

(3) Malipo ni stahili na itapigiwa hesabu kwa kuzingatia masaa ya kazi na si kuzingatia bidhaa zilizozalishwa na mwanagenzi.

(4) Malipo yatalipwa kifedha tu na hayatajumuisha aina nyigine ya malipo.

Kukiukwa mkataba/ makubaliano ya mafunzo ya uanagenzi

2**1.-**(1) Masharti ya sheria nyingine zinazohusika na taratibu yatatumika pale ambapo mkataba umekiukwa kati ya mwanagenzi na mtoa mafunzo.

(2) Pale ambapo makubaliano yamevunjwa na mtoa mafunzo, mwangalizi au mtoto, kwa msaada wa afisa ustawi wa jamii ataomba msaada wa afisa wa kazi au Mahakamani.

## SEHEMU YA SABA
### MAJUKUMU YA MWANAGENZI NA MWANGALIZI

Wajibu wa mwangalizi wa mtoto kutoa taarifa za kunyanyaswa au kuonewa/ kunyonywa

**22.-**(1) Mwangalizi atakuwa na jukumu la kutoa taarifa ya unyanyasaji wowote au udhalilishaji kwa afisa ustawi wa jamii au mamlaka za serikali za mitaa iwapo mwangalizi ana mashaka kuwa kuna unyanyasaji au udhalilishaji.

(2) Mtu mwingine yeyote anaweza kutoa taarifa ya unyanyasi au udhalilishaji kwa Afisa Ustawi wa Jamii au Mamlaka za Serikali za Mitaa pale ambapo mtu ana mashaka kuwa kuna unyanyasaji au udhalilishaji wa mwanagenzi.

(3) Pale ambapo mtoto unyanyasi au udhalilishaji wa Afisa Ustawi wa Jamii au Mamlaka za Serikali za Mitaa pale ambapo mtu ana mashaka kuwa kuna unyanyasaji au udhalilishaji wa mwanagenzi.

Wajibu wa kufuata maelekezo halali

**23.** Mwanagenzi atafuata maelekezo na miongozo halali kwa kadri itakavyoelekezwa na mtoa mafunzo.

Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu uharibifu wa mali

**24.** Mwanagenzi atatoa taarifa ya uharibifu wowote wa mali ya Mtoa mafunzo.

Wajibu wa mtoto kutoa taarifa kuhusu kunyanyaswa au kunyonywa

**25.-**(1) Mtoto hataiba, kuficha au kuchukua mali yeyote ya mtoa mafunzo bila ya ruhusa ya mtoa mafunzo.

(2) Katika nyakati zote, mtoto atahakikisha mafunzo na matumizi bora ya vifaa vya mtoa mafunzo.

Wajibu wa mtoto kutoa taarifa kuhusu kunyanyaswa au kunyonywa

**26.** Mtoto atakuwa na jukumu la kutoa taarifa ya unyanyasaji au udhalilishaji wa Afisa Ustawi wa Jamii, mamlaka za serikali za mitaa au taasisi nyingine yoyote inayoshughulika na haki za watoto.

## SEHEMU YA NANE
### USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI

Wajibu wa Afisa Kazi

**27.-**(1) Litakuwa ni jukumu la Afisa Kazi kukagua mazingira ya kazi na viwango kwa mujibu wa Sheria hii, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria ya Taasisi za Kazi na sheria nyingine yoyote inayohusika pamoja na kanuni zake husika.

(2) Afisa Kazi atakuwa uwezo wa kumhoji mtoto kwenye sehemu ya faragha pasipo mtoa mafunzo kuwepo au mtu mwingine yeyote.

(3) Afisa Kazi atakuwa na uwezo wa kuamarisha mtoto kuachiliwa mara moja kutoka katika uangalizi wa mtoa mafunzo iwapo mazingiara ya mafunzo yataonekana kuwa ni ya unyanyasaji au udhalilishaji.

(4) Pale ambapo Afisa Kazi ametoa amri ya kuachiliwa kwa mwanagenzi kutoka katika uangalizi wa mtoa mafunzo, Afisa huyo wa Kazi mara moja atampeleka mtoto kwenye taasisi inayofaa au kwa Afisa Ustawi wa Jamii.

(5) Afisa Kazi atampatia taarifa mara moja Afisa Ustawi wa Jamii kuhusu kuondolewa katika mafunzo mtoto au kuwaarifu

kuhusu mazingira ya unyanyasaji katika muda usiozidi saa ishirini na nne (24) tangu afanye ukaguzi.

(6) Pale ambapo Afisa Kazi anaamuru mtoto kuachiliwa, Afisa huyo wa Kazi atatakiwa kujaza fomu ili kumtaarifu Afisa Ustawi wa Jamii kuhusiana na hali ya mazingira ya sehemu ya kazi, athari zinazohusika, madhara yaliyopatikana na mapendekezo ya hatua ya kuchukuliwa.

(7) Afisa Kazi atatoa mara moja taarifa ya kutokutekelezwa kwa amri yake na matukio ya kikazi kuhusiana na ajira kwa mtoto kwa mamlaka zilizoidhiniwa kama ilivy oainishwa kwenye Sheria ya Taasisi za Kazi na Kanuni zake.

(8) Afisa Kazi atachukua hatua zote kufuatilia utekelezaji wa Sheria.

Wajibu wa msimamizi wa elimu ya ufundi

**28.-**(1) Mkaguzi wa Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) atachukua hatua zote kufuatilia utekelezaji wa viwango vya mafunzo kwa kutumia nyenzo zilizoidhinishwa na mamlaka ya mafunzo iliyoainishwa.

(2) Mkaguzi wa Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) mara moja atamtaarifu Afisa Kazi iwapo mazingira ya mafunzo ni ya unyanyasaji au udhalilishaji kwa mwanagenzi.

(3) Mkaguzi wa Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) atawajaibika kuhakikisha kuwa wanagenzi waliomaliza mafunzo ya uanagenzi wanapewa vyeti kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET).

Wajibu wa Afisa Ustawi wa Jamii

**29.-**(1) Afisa Ustawi wa Jamii atachukua hatua zote kufuatilia kesi zilizotolewa taarifa kuhusiana na unyanyasaji na udhalilishaji wa wanagenzi.

(2) Iwapo Afisa Ustawi wa Jamii ataona kuwa mwanagenzi anayanyaswa au kudhalilishwa, Afisa huyo atamuondoa mtoto huyo na kutoa taarifa ya suala hilo latika kituo cha polisi na kwa Afisa wa Kazi.

(3) Polisi au Afisa Ustawi wa Jamii atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mtoto aliye kwenye uanagenzi unaonyanyasa au kudhalilisha, anapewa huduma za kumrudisha katika hali ya kawaida.

(4) Afisa Ustawi wa Jamii atawajibika kumfuatilia mwangalizi wa mwanagenzi na kumtaarifu kuhusu kuondolewa

kwa mwanagenzi huyo na kumtaarifu kuhusu mazingira ya kuondolewa huko.

(5) Afisa Ustawi wa Jamii atampatia mwangalizi na mwanagenzi msaada mwingine wowote utakao hitajika ikijumuisha kumpeleka mwangalizi kwenye sehemu ya msaada wa kisheria, husuma ya matibabu na msaada wa kisaikolojia.

Wajibu wa Mkaguzi wa afya na Usalama Mahali pa Kazi

**30.-**(1) Pale ambapo Mkaguzi wa Usalama wa Afya mahali pa kazi anakuta kuwa mwanagenzi ananyanyaswa au kudhalilishwa, afisa huyo atamuondoa mtoto na kutoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii na Afisa Kazi.

(2) Mkaguzi wa Usalama wa Afya mahali pa kazi, atakagua viwango vya usalama wa afya katika sehemu ya mafunzo.

(3) Mkaguzi wa Usalama wa Afya mahali pa kazi atakagua vitendea kazi, ikijumuisha mavazi na vifaa.

## SEHEMU YA TISA
### UTATUZI WA MIGOGORO

Adhabu kwa ukiukwaji

**31**. Pale ambapo mtoa mafunzo anakiuka masharti ya sheria yoyote inayosimamia wanagenzi au Kanuni hizi, adhabu zote zilizotolewa chini ya Sheria hiyo, kwenye kanuni za Adhabu na Sheria nyingine zote husika na Kanuni zitatumika.

Utatuzi wa migogoro

**32.-**(1) Afisa Kazi atashauriana na Afisa Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) wa mkoa na Afisa Usttawi wa Jamii kuhusu kuwasikiliza wahusika na iwapo mazingira yanaruhusu kutatua mgogoro kwa njia ya maelewano.

(2) Iwapo wahusika hawakuridhika na upatanishi, watakuwa na haki ya kufungua kesi kwenye Mahakama.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii atahakikisha kuwa mtoto anapata msaada, ikijumuisha msaada wa kisheria, kiafya na kisaikolojia kama itakavyohitajika.

(4) Katika nyakati zote, Afisa Ustawi wa Jamii ataambatana na mtoto na kuhakiki uwepo wa waangalizi wakati wote wa kipindi cha kusikilizwa kwa shauri.

Dar es Salaam,
27 Machi, 2012

HADJI H. MPONDA,
*Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii*